

07/12/2023

Kumb. Na. MB/SS/HM/01/023

Jina la Mwanafunzi.....

S.L.P.....

YAH**: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MOITA WILAYA YA MONDULI MKOA WA ARUSHA MWAKA 2024.**

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukujulisha kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga **Kidato chaKwanza** katika Shule ya Sekondari Moita Bwawani.
Shule ipo umbali wa kilometa **40** Kusini Magharibi mwa makao makuu ya Wilaya ya Monduli. Kama unatokea Arusha mjini, ipo magharibi mwa Kambi ya J.K.T Oljoro kilometa sita (6) kutoka J.K.T Oljoro hadi Shuleni.

Kama unatokea Monduli mjini, Makuyuni, n.k, unaweza kupata usafiri siku ya Jumanne-Duka bovu na siku ya Jumatano Kisongo. Siku nyingine utapitia Mbauda, **Kwa Morombo** na utapata usafiri mpaka J.K.T Oljoro maarufu kama Jeshi la Pili na ukifika hapo utaona kibao kitakuelekeza na utafika shuleni kwa urahisi.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha orodha ya vifaa muhimu ambavyo lazima mwanao awe navyo. **Sheria za shule hii, kanuni za shule ambazo anatakiwa azifuate kwa muda wote atakaokuwa mwanafunzi wa shule hii, fomu ya uthibitisho wa afya yake, fomu ya taarifa binafsi ambazo anatakiwa kuzikamilisha kabla hajafika shuleni, pamoja na fomu ya kukubali nafasi katika shule hii.**

Kumbuka kipimo cha maendeleo yetu ni taaluma, kazi za nje pamoja na nidhamu ndani na nje ya shule kwa muda wote atakaokuwa shuleni.

NB: - Ni muhimu kwa Mzazi/Mlezi kuzisoma kanuni na sheria za shule na kufuatilia maendeleo ya mwanao ili tushirikiane kumlea mtoto wetu vizuri.

Muhula wa kwanza wa masomo kwa Mwaka 2024 unaanza tarehe 06**/01/2024**na mwisho wa kuripoti ni tarehe **22/01/2024**. Mwanafunzi asiporipoti hadiifikapotarehe**22/01/2024**, Mzazi/Mlezi**atakamatwa**na kuchukuliwa hatua kali za kisheria kwa kumnyima Mtoto haki yake ya msingi ya kupata elimu. **Aidha iwapo utampeleka Mwanao shule ya binafsi, toa taarifa mapema kwa Mkuu wa Shule au katika ofisi ya Afisa Elimu Sekondari ili kuepuka usumbufu wa kukamatwa.**

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1Sare za shule

Sare za Shule hii ni: -

(a) Suruali mbili zarangiyaDark Bluekwaajiliya darasani
(b) Suruali mbili rangi nyeusi kwa ajili ya kazi za nje.

NB: - Mifuko iwe ya kawaida isiwe ya mbele wala nyuma kama jeans.

(c) Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi shonea kitambaa cha rangiyasuruali(Dark Blue) kwenye kola ya shati kwa nyuma, na hapo paliposhonwa patariziwe herufi za jina la mwanao.
(d) Tai mbili zarangiyaDark Blue.
(e) Sweta moja la rangi**Dark Blue**
(f) T – shirt mojayarangiDark Blueyenye kola(form six)utaratibu wa tshrt,rangi na nembo utapatikana shuleni.
(g) Soksi jozi mbili (2) rangiya**Nyeusi**
(h) Bukta (2) rangiya**Dark Blue**kwaajiliya michezo
(i) Raba kwa ajili ya michezo
(j) Viatu vya ngozi vyeusi (vyenye kamba) pea mbili, visiwe na visigino virefu,
(k) Mkanda (wa ngozi) rangi **nyeusi**
(l) Mabuti pea (1) kwa ajili ya matope.
(m) Track suit yarangiDark Blueyenye**upindomweupe pembeni.**
(n) **Pull neck yaDark Blue**mojakwaajili ya kujikinga nyakati za baridi.

2.2 Malazi-Vifaa: -

Unatakiwa kuja na vifaa vya kulalia kama ifuatavyo: -

(a) Godoro aina ya **Tanform futi** mbili na nusu kwa sita ($2^1/_2$ x 6) lenye kava.
(b) Blanketi (1)
(c) Mashuka mawili (2) rangiya DARK BLUE
(d) Mto wa foronya
(e) Chandarua (Mosquito net)

2.3 Vifaa vya Chakula

a) Sahani ya chakula (Ya Aluminium)
b) Kijiko
c) Kikombe (Cha Aluminium)
d) Bakuli ya uji (Ya Aluminium).

2.4 Mahitaji mengine

(a) Ndoombili (2) yaplastikiyalita 10 kwaajiliyakuogea nay a majiya kunywa.
(b) Taulo moja (1)
(c) Sanduku imara (la chuma) lenye kufuli.
(d) Madaftari kumi makubwa (counter books).
(e) Vifaa vya hisabati (mathematical set)
(f) File moja la nailoni kwa ajili ya kutunzia mitihani yake.
(g) Jembe moja lenye mpini imara.
(h) 'Ream' ya karatasi (**plain papers A4**) yake binafsi za kufanyia majaribio kila Jumatatu ya juma (**weekly test**)
(i) Kadi yake ya bima ya afya (NHIF, CHF) na kama hana kadi yoyote itampasa aje na Tsh 6000/- kwa ajili ya kukatiwa Bima ya Afya shuleni.

<u>ZINGATIA</u>: Ni muhimu sare zote za shule na vifaa vya malazi viandikwe majina ya mwanao na vifaa vingine vyote viwekwe alama ambayo haifutiki.

3.0Sheria Na Kanuni Muhimu Za Shule Hii.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na-25 ya mwaka 1978 na ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi, Teknolojia na Ufundi Mafunzo, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya RAISI-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Kutunza mali za Umma
(j) Mavazi yasiyostahili kama, makoti, majaketi, kofia ni marufuku.
(k) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na mali ya thamani kama simu, kamera n.k
(l) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na silaha ya aina yoyote.

3.1 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Ukafukuzwa Shule Mara Moja.

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kusababisha mimba.
9. Kuoa / kuolewa
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kumiliki na kutumia simu
14. Kusababisha mimba ndani na nje ya shule
15. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya mkuu wa shule
16. Kutohudhuria shule kwa siku 90 kwa muhula.

3.2 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa Shuleni na Mwanafunzi

(a) Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

3.3 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NIDHAMU, TAALUMA NA KUJITUMA NDIO VIPAUMBELE VYETU.

……
NEHEMIAH MBOYA
0755 521 655
MKUU WA SHULE.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI
MAWASILIANO
MKUU WA SHULE,
0755 52 16 55
0672 55 26 55
MOITA SEC SCHOOL
P.O.BOX 161
MONDULI
ARUSHA
EDUCATION IS POWER

Date……

MEDICAL EXAMINATION FORM

TO MEDICAL OFFICER,
……
……
……..

PART A:

Mr/Miss ……

Please examine the above named pupil to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following:

1. Haemoglobin …….....
2. P.V. Bleeding …….....
3. Sight …….....
4. Blood pressure …….....
5. Urine for sugar …….....
6. Stool for routine examination …….....
7. Asthma …….....
8. Skin diseases …….....
9. Leprosy.....
10. Any deformity.....
11. Epilepsy.....
12. Pulmonary tuberculosis …….....
13. Neurosis ……..…….....
14. General diseases ……..…….....

PART B:

MEDICAL CERTIFICATION

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named pupil and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit to join the school.

……

Signature (Dr.)

FOMU YA KUKUBALI

1. Mimi……nimekubali kuingia kidato cha ……
katika shule ya sekondari Moita kama mwanafunzi wa Bweni. Ninaahidi nitafika shuleni bila kuchelewa.
2. Ninaahidi kuwa Nitatii sheria za shule, sitajihusisha wala kuchochea mgomo wakati wote niwapo shuleni.
3. Ninaahidi kuwa Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea.

Saini ya mwanafunzi …….....tarehe …….

SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI:

1. Mimi ……nimekubali mtoto wangu……asome katika shule ya Sekondari Moita kuanzia tarehe ……
2. Ninaahidi kumpa vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua.
3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi nyinginezo za kujitegemea.
4. Ninakuhakikishia kwamba mtoto wangu hatachelewa kurudi shuleni pindi apatapo likizo fupi au ndefu, atafika kwa muda unaotakiwa.
5. Anwani yangu ya kudumu ni:
……
……..
Namba ya simu ya Baba……. Namba ya simu ya mama ……
Namba ya simu ya Kaka…… Namba ya simu ya dada…….
Namba ya simu ya mlezi……

6. Saini ……